

102/3

KISWAHILI

Fasihi

Karatasi ya 3

Muda : Saa 2 ½

KIDATO CHA 3

Hati ya kuhitimu kisomo Secondary Kenya(KCSE)

KISWAHILI

Karatasi ya 3

MAAGIZO:

- *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
- *Jibu maswali manne pekee.*
- *Swali la kwanza ni lazima.*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizosalia yaani; (Riwaya, Hadithi fupi, Tamthiliai na, fasihi simulizi.*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*
- *Kila swali lina alama 20*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI :-

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	80	

Karatasi hii ina kurasa 3 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

SEHEMU YA A: USHAIRI

SWALI LA LAZIMA

Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo

MKULIMA

Mtazameni ...nguzo ya Afrika

Mtumwa wa watumwa waloridhiya!
Amekita jembe lake akilisujudia
Kwa tambo lililoumbuka na kuselehea
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia
Na machungu ya maonevu alovumilia

Moyo wake nzito ulikomaa kama kuni
Haujui tena kutarajia wala kutamani
Umekufa ganzi, kutoishi wala huzuni

Basi iteni fikira mambo mukiyafikiri
Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari
Siku ukweli na hali yake utapodhihiri
Umejiandalilia vipi....

huo mkono ulomuumbua na kumkausha
hizo pumzi zilizomzimia taa ya maisha
humfunga kizuizini, gizani *kumtowesha?*

Ni jawabu gani aliwekewa na wakati
Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti
Kuliwaza hamaki ya njaa hii ya dhati
Njaa ya maisha itakayo kushibishwa

Maswali

- (a) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shairi hili (al.4)
- (b) Taja na utoe mifano za aina zozote **mbili** za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili (al.4)
- (c) Eleza umbo la shairi hili (al.2)
- (d) Onyesha umuhimu wa matumizi ya kihisishi katika shairi (al.2)
- (e) Fafanua maana ya:
- (i) Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari (al.2)
- (ii) Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti (al.2)
- (f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi (al.3)
- (i) tambo
- (ii) ulokomaa

(iii) kumtoweka

SEHEMU YA B: RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA: Ken Walibora

2. Uzembe na mapuuzza huathiri maendelo ya nchi. Thibitisha (al.20)
3. Ninyi ni ndugu? Naona mna mshabaha.....
- (i) Eleza muktadha wa dondoo hili? (al.4)
- (ii) Mzungumzaji alikuwa mhusika wa sifa kandamizi. Eleza (al.10)
- (iii) Wanaozungumziwa walikumbana na dhiki nyingi maishani mwao. Eleza kwa kutoa mifano (al.6)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA

MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE

4. Jina si kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa yako
- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
- (b) Fafanua jinsi tumbo limewekwa mbele ya jina katika tamthilia hii (al. 16)
5. Ufisadi unaendelezwa na Baraza. Eleza (al.20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI: (KEN WALIBORA NA SAIDI A. MOHAMMED)

6. Ni matatizo gani yanayowakumba vijana wanaoenda masomoni ughaibuni Fafanua kwa kurejelea hadithi ya Damu Nyeusi (al.20)

SEHEMU YA E

7. FASIHI SIMULIZI

- (a) Eleza umuhimu wa aina zifuatazo za ngano katika jamii
- (i) Ngano za mtanziko (al.6)
- (ii) Fafanua umuhimu wa maigizo ya watoto (al.6)
- (iii) Fafanua sifa **tano** za RARA (al.5)
- (iv) Eleza dhima ya misimu kama kipera cha usemi (al.4)